JAMHURI YA MUUNGANOWA TANZANIA

OFISIYARAIS

TAWALAZAMIKOANASERIKALIZAMITAA

# MAELEKEZO YAKUJIUNGA NAKIDATOCNATANOKATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

April,2024

Dodoma

JAMHURIYAMUUNGANOWATANZANIA

OFISIYARAIS—TAMISEMI

Namba za Simu

Mkuu wa Shule,0764876455

Makamu Mkuu wa Shule, 0745905369

MatronlPatron,0762575544,0766305472

Shule ya Sekondari MAZWI

S.L.P.632

Tarehe 19/04/2024

Mzazi/Mlezi waMwanafunzi.............

S.L.P...........................................

Yah:MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MAZWI HALMASHAURI YA SUMBAWANGA MKOA RUKWA MWAKA 2024/2025

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2024/2025 na atasoma tahasusi ya HGK/HKL/HGFa

Shule ya Sekondari Mazwi ni Kutwa na ipo umbali wa Mita 5 Kusini mwa stendi kuu ya mabasi (stendiyasokomatola) katika Mji wa Sumbawanga

2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

Sare za Shule

i) a) Wasichana: Sketi mbili(2), Moja damu ya mzee na nyingine dark bluu

b) Wavulana: Suruali mbili (2), Moja damu ya mzee na nyingine dark bluu

ii. Shati mikono mirefu nyeupe mbili(2)

iii) Rangi ya Hijab (kijuba),(ifanane na rangi ya sketi) ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama

iv) Vazi la tai iendane na sketi na suruali .

v) Sare ya Michezo ni traki suti, rangi ya bluu bahari yenye ufito mweupe, kwa wasichana na wavulana na raba jozi moja Kwa wasichana na wavulana

vi) Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;

vii) Soksi jozi mbili rangi nyeupe

viii) Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali

ix) Sweta rangi ya Dark bluu

x) Tisheti (T-shirt) zitapatika hapa shuleni

Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja Nayo shuleni:-

i. Madaftari kumi(10) ziwe kwaya 3 na zaidi;
ii. Ream(A4) ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika(kwa ajili ya kujisomea).
iv. Ndoo1 ndogo (litaKumi) yenye mfuniko
v. Kwanja 1,jembe1, reki1,mfagio 1(mgumu).

Michango mbalimbali

| Na | AinayaMchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchangowa Uendesha wa Shule | 35,000/— |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | KitambulishochaShule | 5000/= |
| | Jumla | 50,000/= |

Michango yote ilipwe kwenye akaunti ya shule ambayo ni
JINA LA AKAUNTI: ELIMU YA KUJITEGEMEA MAZWI SEKONDARI
AKAUNTI NAMBA : 62102300019 (NMB)

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais —TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo nipamoja na;

### Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo Ia lazima
ii Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shulekulingana na ratiba ya shule;
i"ti Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
iV. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
V. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
Vi. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
vii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
Viil. Kutunza mali za shule;
ix Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
X. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni

MUHIMU:

- Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwanamna yoyote ile,na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;

•'Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule.(Msiba au Ugonjwa)

Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwazaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro,
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake,walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. v Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
i Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni au kusuka kwa mtindo wa ususi uliokubalikana uongozi wa shule;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsia moja,kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki,kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua,au kutishia kujiua kama kunywa sumu;na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi

4. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (MedicalExaminationForm) ambayo itajazwa na Mganga MKuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria kanuni na maełekezo mengine yanayotolewa na shulena

IV.Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu

v) Aje na matokeo ya kidato cha nne (result slip)

5. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

KARIBU SANA KATIKA SHULE HII

Saini ya Mkuu wa Shule................................

Jina la Mkuu wa Shule GODSON G MWAIBINGILA

Mhuri wa Mkuu wa Shule ................................ THE HEADMASTE ... SECONDARY SCHOOL ...AZWI ... SUMBAWANGA

hlB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husikaambayeni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE,NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -

Mkuu wa shule 0764876455

Makamu Mkuu wa Shule 0745905369

Mwandamizi Taaluma 0628141813

MwandamiziMalezi 0753800123